# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Aprili, 2024**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu 0788744141**

**Mkuu wa Shule 0788744141**

**Makamu Mkuu wa Shule 0694182313/0789650813**

**Matron/Patron.................0787320758**

**Shule ya Sekondari Endasak**

**S.L.P 145**

**Tarehe 26/04/2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**………………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI ENDASAK HALMASHAURI YA HANANG MKOA MANYARA MWAKA 2024/2025**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024/2025 na atasoma tahasusi ya EGM/PCM/PCB/HKL/HGLi

Shule ya Sekondari Endasak ipo katika Halmashauri ya (W) Hanang, Mkoa wa Manyara, na shule hii ipo umbali wa kilometa ishirini (20km) kutoka makao makuu ya Wilaya Mashariki mwa mji wa Katesh. Kwa wanaotoka Singida – Arusha watashukia mji mdogo wa Endasak km20 kutoka makao makuu ya Wilaya. Kutoka Mji mdogo wa Endasak shule ipo umbali wa kilometa 0.8 Nauli sh. 1,000/= kwa usafiri wa bodaboda au unaweza kufika kwa miguu.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 01/07/2024 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 01/07/2024 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 15/07/2024

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:**

**2.1 Sare ya shule.**

**(a) Wasichana:**

**(i) Sare ya darasani:**

- Sketi mbili (2) **Rangi ya orange(Karoti)** kitambaa kizito, mshono wa heshima yenye marinda ya upanga 12**. (Mbele rinda sita na nyuma rinda sita.)** zipu ikiwa pembeni kushoto na mfuko kulia. Kitambaa kiwe kikubwa kinachoruhusu sketi iwe nzuri yenye kujimwaga hadi chini. Urefu wa sketi ufike kwenye kifundo cha mguu ,Sketi fupi hairuhusiwi shuieni. 'Belt' ni inchi mbili (2) na pindo la chini liwe la wastani.
- Mashati meupe mawili ya tetron yenye mikono mirefu.
- Tai 'dark blue', fupi kiasi na pana pamoja na pini yake.
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na visigino vifupi.
- Sweta rangi ya 'dark blue shingo 'V'
- Soksi ndefu nyeupe jozi mbili.
- *Iwapo mwanafunzi ni mwislamu rangi ya* Hijabu (kijuba) ni nyeupe mbili (2) isiyo na marembo yoyote. Ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

**(b) Wavulana:**

- Suruali mbili (2) rangi ya kaki, kitambaa kizito, mshono wa heshima, iwe marinda mawili mbele (celebration) upana wa chini nchi 17 na pindo la 'turn up'.
- Mashati meupe mawili ya tetron yenye mikono mirefu.
- Tai ya 'dark blue' fupi kiasi na pana pamoja na pini yake.
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na visigino vifupi.

- Sweta rangi ya ‘dark blue’ shingo ‘V’.
- Soksi za kaki ndefu jozi mbili.
- Mkanda mweusi wa ngozi wakufalia suruali.

**(ii) Mavazi ya kazi (shamba dress)**

**(a) Wasichana.**

- Gauni (2) rangi ya ugoro na mshono; shingo ya duara mikono mirefu marinda box mbele na nyuma iwe na mikanda ya kufunga nyuma,urefu mpaka kwenye kifundo cha mguu.
- Iwapo mwanafunzi ni mwislamu rangi ya Hijabu (kijuba) ni ugoro mbili (2) isiyo na marembo yoyote. Ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

- Awe na raba nyeupe au nyeusi (**mwanafunzi haruhusiwi kuvaa ndala nje ya bweni au darasani)**. **Ndala zitatumika ndani ya bweni tu kwa matumizi ya kuoga.**

- **Awe na mabuti ya mvua meusi au kijani jozi moja.**

-Vazi la kazi litavaliwa na sweta rangi ya ugoro lenye shingo v

-Tshit za kazi mbili (2) rangi ya kijani yenye kola. Kwa mzazi atakayeshidwa kupata t-shit, zinapatikana shuleni kwa @SH.15,000/=

**(iii) Wavulana.**

- Suruali mbili (2) rangi ya ugoro nzito mshono kama suruali za darasani.
- Mabuti ya mvua meusi au kijani jozi moja tu.
- Mwavuli moja (1) kwa wote kwa ajili ya kujikinga na mvua kipindi cha masika.
- Raba nyeupe au nyeusi **(mwanafunzi haruhusiwi kuvaa ndala nje ya bweni au darasani). Ndala zitatumika ndani ya bweni tu kwa matumizi ya kuoga.**

-Vazi la kazi litavaliwa na sweta rangi ya ugoro lenye shingo ya v

- Tshit za kazi mbili (2) rangi ya kijani yenye kola. Kwa mzazi atakayeshidwa kupata t-shirt, zinapatikana shuleni kwa @SH.15,000/=

**(iv) Sare za michezo.**

Kila mwanafunzi anatakiwa kushiriki michezo. Michezo ni lazima na ni somo mojawapo linalotiliwa mkazo na kuthaminiwa sana hapa shuleni.

Hivyo mwanafunzi itamlazimu aje na nguo za michezo ili kufanikisha shughuli za michezo kama ifuatavyo:-

**(a) Wasichana:**

- T-Shirt rangi nyeusi yenye michirizi nyeupe na bukta nyeusi yenye michirizi ya nyeupe kwa tahasusi ya HKL
- T-shirt rangi nyekundu yenye michirizi nyeupe pamoja bukta yake kwa tahasusi ya PCB
- T-shirt rangi ya bluu yenye michirizi nyeupe na bukta yake kwa tahasusi ya PCM
- T-shirt rangi ya kijani yenye michirizi nyeupe na bukta yake kwa tahasusi ya HGLi
- T-shirt rangi ya njano yenye michirizi nyeupe na bukta yake kwa tahasusi ya EGM.
- Track suit rangi ya blue (**ISIWE NA KOFIA**).
- Raba jozi moja (1) za michezo 'njumu'.
- Soksi za michezo jozi mbili (2).

**(b) Wavulana.**

- T-Shirt rangi nyeusi yenye michirizi nyeupe na bukta nyeusi yenye michirizi ya nyeupe kwa tahasusi ya HKL
- T-shirt rangi nyekundu yenye michirizi nyeupe pamoja bukta yake kwa tahasusi ya PCB
- T-shirt rangi ya bluu yenye michirizi nyeupe na bukta yake kwa tahasusi ya PCM
- T-shirt rangi ya kijani yenye michirizi nyeupe na bukta yake kwa tahasusi ya HGLi
- T-shirt rangi ya njano yenye michirizi nyeupe na bukta yake kwa tahasusi ya EGM
- Track suiti rangi ya blue (**ISIWE NA KOFIA**).
- Raba jozi moja (1) za michezo 'njumu'.
- Soksi za michezo jozi mbili (2).

**(v) Mavazi kwa ajili ya kuzuia baridi (nje ya darasa) wavulana na wasichana.**

- 'Pull neck' mbili (2) nyeupe zisizo na maandishi wala madoido yoyote.

➢ ***MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUJA NA NGUO ZA NYUMBANI.***

**2.2Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 12 (*Q4*);

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*Vimeambatanishwa*);
iv. Koti Jeupe la mahabara kwa wanafunzi wa PCM&PCB
v. Scientific Calculator;
vi. Aje na godoro moja inchi 2 ½ x 3 x 6.
vii. Mashuka jozi 2 rangi ya blue bahari, blanketi 1, foronya 2 rangi ya blue bahari pamoja na mto wa kulalia 1, chandarua 1 nyeupe au blue pembe nne au duara. Aje na taulo, nguo za kulalia mbili (2), sanduku moja la chuma (tranka) moja tu lenye kufuli imara
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 (soft brum na chelewa) wa ndani na nje na ndoo 1 kwa tahasusi ya EGM,PCM na HKL kwa tahasusi ya PCB na HGLi atakuja na mkasi 1 wa kukatia maua,fagio 1 ya chelewa,ndoo 1 ya lita 20.
xii. Bima ya afya au uje na 50,400 kwaajili ya kukuta bima ya afya au waweza kukatia huko ulipo kwenye ofisi za bima za halmashauri.

**2.3 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB:** Michango yote ilipwe kwenye akaunti ya shule **Na. 41001200079** katika benki ya **NMB** Tawi lolote nchini, jina la mwenye akaunti ni **Endasak Secondary.** Mwanafunzi atatakiwa kuleta 'Bank Pay In Slip' **(BPS)** iliyoandikwa jina kamili la mwanafunzi yeye mwenyewe na si jina la mzazi, mlezi au aliyetuma fedha.

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa.Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule nipamojana:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wotewawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.
v. Nakala halisi (original) vya vyeti vya kitaaluma pamoja na vivuli vya vyeti hivyo (Result slip,leaving certificate na cheti cha kuzaliwa)

**5**. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ……………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule …………………………………….**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0788744141**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0694182313/0789650813**
- **Mwandamizi Taaluma 0786497695/0759315694**
- **Mwandamizi Malezi 0789761441/0789529949**

**ORISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**KIAMBATISHO ‘A’**

**SHULE YA SEKONDARI ENDASAK**
**FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA SHULE PAMOJA NA MASHARTI YAKE MWAKA 2023/2024:**

**A: MWANAFUNZI:**

Mimi …………………………………………………………………………….nimesoma kwa makini maagizo ya kujiunga na shule ya sekondari Endasak, pia nimesoma na kuelewa vema sheria za shule. Kwa heshima na taadhima na unyenyekevu mkubwa ninakubali/sikubali nafasi hiyo pamoja na masharti na sheria za shule kwa sababu :-
(**iwapo unakubali nafasi hii toa sababu vivyo hivyo kama unakataa nafasi hii toa sababu).**

……………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………

Tarehe ……………………………………………………        Saini
………………………………………………

**B: MZAZI/MLEZI:**

Mimi ………………………………………………………………………Mzazi/Mlezi wa ………………………………………… Ambaye amechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari Endasak, nimesoma kwa makini maagizo ya shule na sheria zake na kuzielewa vema. Ninakubali/ninakataa nafasi hiyo, ninaahidi/siahidi kumimizia mtoto wangu mahitaji na maagizo yote ya kujiunga na shule kwa muda uliopangwa.
Aidha naahidi/siahidi kushirikiana daima na uongozi wa shule katika kumkuza, kumlea mtoto huyu kwa manufaa yake binafsi, wazazi, jamii na Taifa kwa ujumla. Kama unakataa eleza sababu:-

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………….

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………….

Ahsante,

(i). Jina la mzaz*/mlezi wa kiume ………………………………….. (ii) Jina la mzazi/mlezi wa kike ………………..
Anwani ……………………………………………………………… Anwani
……………………………………………………… Namba ya simu ya mkononi
…………………………… Na. ya simu ya mkononi …………………………..
Tarehe ……………………… Saini ………………………….
Tarehe……………………… Saini …………………….

**Ndugu/*jamaa (3) watatu watakaoruhusiwa kumtembelea mtoto/mwanafunzi nje ya wazazi/walezi.**
**N.B. Ndugu na jamaa watakaothibitishwa hawatahusika katika maamuzi ya masuala ya kinidhamu ya mwanafunzi.**

Mimi *mzazi/mlezi nathibitisha kuwa waliojiandikisha hapo chini ni ndugu *zangu/jamaa wa karibu ambao wanaweza kuruhusiwa kumtembelea mtoto wangu na siyo vinginevyo.
Jina la mzazi/mlezi ……………………………………… Saini ……………………………………

| **S/N** | **MAJINA MATATU** | **UHUSIANO WAKE NA MTOTO** | **ANWANI** | **SIMU YA MKONONI** | **SAINI** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | |
| 2. | | | | | |
| 3. | | | | | |

*Kata lisilohusika.
NB. Sehemu ‘B’ ijazwe na kusainiwa na mzazi/mlezi na si vinginevyo.

……………………………….
**Gisela A. Msoffe (<u>MKUU WA SHULE</u>)**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENT OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**KIAMBATISHO ‘B’**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**
**ENDASAK SECONDARY SCHOOL**
**P.O. BOX 145,**
**KATESH – HANANG,**
**MANYARA.**

**REF. No. ESS/ME/VOL. I/………….. DATE ………………………………..**

**TO THE MEDICAL OFFICER,**
**……………………………………………………….**
**………………………………………………………. (GOVERNMENT HOSPITAL)**

STUDENT’S NAME ……………………………………………………………….AGE……….YEAR……………
Please examine the above named student and arrange for any necessary treatment for student if need be.

…………………………………………….

Gisela A.Msoffe
THE HEAD OF SCHOOL

MEDICAL CERTIFICATE:
(To be completed by the medical officer)
I have examined the above named with regard to:
Skin
………………………………………………………………………………………………………………..
Eyes
……………………………………………………………………………………………………………………
Ears
……………………………………………………………………………………………………………………
Teeth
………………………………………………………………………………………………………………..
B/S Test (Chronic)
………………………………………………………………………………………………..
Pressure
……………………………………………………………………………………………………………
Abdomen
…………………………………………………………………………………………………………
Chest
………………………………………………………………………………………………………………..
Stomach
……………………………………………………………………………………………………………
Urine
…………………………………………………………………………………………………………………
HB. Haemoglobin
…………………………………………………………………………………………………
TB Test
………………………………………………………………………………………………………………
VDRL
…………………………………………………………………………………………………………………
HIV Test
……………………………………………………………………………………………………………

UPT Test
………………………………………………………………………………………………………
……
Stool
………………………………………………………………………………………………………
…………
Ulcers
………………………………………………………………………………………………………
………
Diabetic
………………………………………………………………………………………………………
……..
Asthmatic
……………………………………………………………………………………………………..
Disabilities (If any)
………………………………………………………………………………………..
Allergies (If any)
…………………………………………………………………………………………………
ADDITIONAL INFORMATION
E.g. Any physical effects or impartment infections, chronic of family disease etc.

1. The student is in good health free from infection diseases and is fit to proceed with studies.
2. The student will be attending treatment for
   ………………………………………………………………………………..
   SIGNATURE ………………………………………………………………..
   DESIGNATION ………………………………………………………….
   STATION ……………………………………………………………………..
   **NOTE: MEDICAL OFFICER**
   *At the time of Examination, please treat the individual for any ailment you note.*

KIAMBATISH
O 'C'

**ORODHA YA MAJINA YA VITABU VINAVYOTAKIWA KUSOMWA NA WANAFUNZI WA KIDATO CHA TANO NA SITA:**

**PHYSICS**

| **NA.** | |
|---|---|
| 1 | S. CHAND'S CLASS XI |
| 2 | S. CHAND'S CLASS XII |
| 3 | ROGER MUNCASTER |
| 4 | UNIVERSITY PHYSICS (UP) |
| 5 | TOM DANCEN |
| 6 | NELKOW & PARKER (7TH EDITION) |
| 7 | COMPRISIVE PHYSICS CLASS XII |

| | |
|---|---|
| 8 | PHYSIC REVIEW (NECTA) |
| | **TOTAL** |
| | **ECONOMICS** |
| 1 | SIMPLIFIER ECONOMICS |
| 2 | ZISTI ECONOMICS I |
| 3 | ZISTI ECONOMICS III |
| 4 | AMBILIKILE ECONOMICS I |
| 5 | AMBILIKILE ECONOMICS II |
| 6 | REVIEW NECTA ECONOMICS I |
| 7 | REVIEW NECTA ECONOMICS II |
| | MODERN ECONOMICS (Robert Mudida ) |
| | **TOTAL** |
| | **ADV. MATHEMATICS** |
| 1 | ADVANCED LEVEL PURE MATHEMATICS - BY C.J. TRANTER |
| 2 | MATHEMATICS FOR CLASS XII VOLUME II WITHVALUE BASED QUESTIONS - BY PURE MATHEMATICS |
| 3 | CAMBRIDGE UNIVERSITY PRES PURE MATHEMATICS TICS |
| 4 | MATHEMATICS AND STATISTICS CONDERSTANDING PURE MATHEMATICS - BY SAOLER |
| 5 | PURE MATHEMATICS 1 - BY BACKHOUSE |
| 6 | PURE MATHEMATICS 2 - BY BACKHOUSE |
| 7 | ADVANCED MATHEMATICS REVIEW FORPAPER 1 (CURRENT) |
| 8 | ADVANCED MATHEMATICS REVIEW FOR PAPER 2 (CURRENT) |
| 9 | APPLIED BASIC MATHEMATICS |
| | **TOTAL** |
| | |
| | **CHEMISTRY:** |
| 1 | CHEMISTRY REVIEW (CURRENTS) PAPER 1 & 2) |
| 2 | ADVANCED CHEMISTRY 4TH EDD, MICHAEL CHIGSTON, RASALIND |
| 3 | S. CHAND'S XII (CHEMISTRY) |
| 4 | RAMSDEN'S |
| 5 | UNDERSTANDING CHEMISTRY |
| 6 | ESSENTIAL CHEMISTRY - S. CHAND'S PHYSICAL CHEMISTRY, CAMBRIDGE |
| 7 | WORK OUT CHEMITRY |
| 8 | INORGANIC CHEMISTRY (S.C. CHAND'S) |

| | |
|---|---|
| 9 | ADVANCED PRACTICAL (F 8c 6) |
| 10 | RAMSDEN CALCULATION (QUESTIONS AND ANSWERS) |
| 11 | ORGANIC CHEMISTRY (S. CHAND'S) |
| 12 | GENERAL CHEMISTRY 5TH EDDITION |
| | **TOTAL** |
| | **GEOGRAPHY 2** |
| 1 | ADVANCED LEVEL PAPER 2 - GEOGRAPHY |
| 2 | HUMAN AND ECONOMIC GEOGRAPHY, LONDON: O.U.P - Morgan, G.C. & Goh Cheng, L (1984) |
| 3 | |
| 4 | GEOGRAPHY OF AFRICA, LONDON: Macmillan publisher - Minns, W.J. (1984) |
| 5 | SUCCESS IN GEOGRAPHY: CLIMATOLOGY AND SOIL SCIENCE, - Dar Es Salaam Afroplus industires Ltd. (Msabila D.T. (2003) |
| 6 | SUCCESSION EXAMINATIONS: GEOGRAPHY PAPER TWO QUESTIONS & ANSWER). Mzumbe Internal printers - Msabila D.T. (2004) |
| 7 | LAND, WORK AND RESOURCES; AN INTRODUCTION TO ECONOMIC GEOGRAPHY. LONDON: Edward Annold, Peterson, J.H. (2006) |
| 8 | AFRICA - A STUDY GEOGRAPHY FOR ADVANCED STUDENTS. London Longman - Pritchard, J.M. (1979) |
| | **TOTAL** |
| | GEOGRAPHY ADVANCED LEVEL PAPER – 1 |
| 1 | TIE 1st EDDITION (2016) - GEOGRAPHY FOR SECONDARY SCHOOLS FORM FIVE. - Dar es Salaam, Tanzania |
| 2 | PHYSICAL GEOGRAPHY IN DIAGRAMS, LONGMAN - R.B. Bunnet (2000). |
| 3 | PRACTICAL GEOGRAPHY FOR AFRICA, Hong Kong, - Pricharch J.M. (1979) |
| 4 | AFRICA IN FOCUS, A PHYSICAL HUMAN AND ECONOMIC GEOGRAPHY - Richard White (1984) |

HISTORY

i. Major in Africa history
ii. Major events in Africa and imperialism
iii. Africa since 1800
iv. Advanced history paper 1 and paper 2- by YASIN

KISWAHILI

i. Sarufi ya Kiswahili-TIE

ii.Vitabu vya fasihi andishi

-ushauri

-kimbunga

-chungu tamu

-mapenzi bora

iii. RIWAYA

-vuta N'kuvute

-mfadhili-

Usiku utakapokwisha

-kufikirika

TAMTHILIA

-Morani

-kivuli kinaishi

-Nguzo mama

-kwenye ukingo wa Thim

ENGLISH LANGUAGE

i.English for A LEVEL Proctical Approach Form Five And Form Six

ii.English language for A LEVEL 5& 6